

Upimaji wa COVID-19

Upimaji wa COVID-19 sasa unapatikana Minnesota.

Video hii inaelezea ni nani anayeweza kupimwa, eneo la kupimiwa na jinsi ya kupata matokeo yako.

Ni nani anayeweza kupimwa COVID-19?

Watu ambao wana dalili za COVID-19 wanapaswa kupimwa.

Dalili zinaweza kujumuisha homa ya joto, kikohozi, upungufu wa pumzi, maumivu ya misuli, kuumwa na kichwa, koo kavu, baridi au kupoteza uwezo wa kuhisi ladha au harufu.

Zungumza na daktari wako, kliniki ya eneo lako au utembelee ramani ya mtandaoni ya maeneo ya kupimiwa kwenye tovuti ya kukabiliana na COVID ya Minnesota ili uweze kutambua ikiwa unahitaji kupimwa. Pata usaidizi kutoka kwa familia, marafiki au wasaidizi wengine ikiwa hujui jinsi ya kutumia tovuti.

Ninaweza kupimiwa wapi?

Kliniki na hospitali nyingi zinaweza kukusanya sampuli kwa ajili ya upimaji kwenye maabara.

Ili upate mahali unapoweza kupimiwa, pigia daktari wako, kliniki ya eneo lako au utembelee ramani ya mtandaoni ya maeneo ya kupimiwa kwenye tovuti ya kukabiliana na COVID ya Minnesota. Pata usaidizi kutoka kwa familia, marafiki au wasaidizi wengine ikiwa hujui jinsi ya kutumia tovuti.

Kabla ya kwenda katika eneo la kupimiwa, piga simu kwanza au upitie maagizo katika ramani ya maeneo maalum ya upimaji kwa sababu yote hayafanani.

Je, nitapataje matokeo ya kipimo changu?

Kliniki iliyofanya kipimo chako itawasiliana nawe ili ikupe matokeo yako.

Hii inaweza kuchukua siku kadhaa.

Usiwasiliane na Idara ya Afya ya Minnesota ili kupata matokeo yako ya maabara.

Ili utumie kifaa cha kujichunguza mtandaoni au kutumia ramani mwingiliano ya maeneo ya upimaji, tembelea mn.gov/covid19

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

05/26/20

Testing for COVID-19 (Swahili)

To obtain this information in a different format, call: 651-201-4989